# KATIBA

# YA

# TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEA)

**JULAI 16, 2021**

**DAR-ES-SALAAM, TANZANIA**

**UTANGULIZI**

Sisi waanzilishi na viongozi wa Taasisi ya TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEA) tumekubaliana kuwa na katiba itakayoongoza mwenendo mzima wa shughuli zetu.

Tumetambua kuwa uhusiano wetu,matatizo na migongano ambayo hutokea katika Taasisi mbalimbali ni matokeo ya kutokufuata kanuni elekezi tangu kuanzishwa kwa Taasisi hizo , Hivyo tumeitunga katiba hii kuendana na sheria za nchi yetu ya Jamhuri ya MuunganoTanzania kuyaondoa kabisa mapungufu yaliyopo na kuleta umoja na mshikamano wenye nguvu katika Jumuiya yetu ndani na nje ya TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEA)kwa kufuata kikamilifu misingi ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA HIYO BASI, TUMEUNDA CHOMBO cha kuhimiza, kuratibu, kusimamia, kushauri, kuhakikisha utekelezaji bora na kushirikisha wanajumuiyakatika SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KIJAMII KWA UJUMLA.

**IBARA YA 1:JINA LA TAASISI**

Jina kamili ni Taasisi ya TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION kwa kifupi ni (TANCEA)

**IBARA YA 2: ANUANI NA MAHALI ILIPO OFISI**

a) Anwani itakuwa Sanduku la Posta 11430 KITUNDA RELINI- Dar-es-Salaam.

b) Ofisi Kuu itakuwa katika mtaa waKitunda Relini mkoa wa Dar-es-Salaam, Nyumba Namba 49H, hata hivyo Viongozi wanaweza kutafuta ofisi sehemu nyengine yeyote.

**IBARA YA 3: MAKAO MAKUU**

Makao makuu yatakuwamtaa wa Kitunda Relini,kata ya Kitunda, wilaya ya Ilala mkoa wa Dar-es-Salaam, Nyumba Namba 49H, hata hivyo Viongozi wanaweza kutafuta ofisi sehemu nyengine yeyote.

**IBARA YA 4:**

**A) LUGHA RASMI**

Lugha rasmi itakayotumika ni Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza ni lugha za ziada.

**B) TAFSIRI YA MANENO**

Katika katiba hii baadhi ya maneno yametumika na kutakuwa na maana mahususi yaliyomaanisha kama:

**WAANZILISHI-** wanzilishi ni wale ambao walikuwepo ambapo Taasisi hii inaanzishwa.

**TANCEA-**Itamaanisha TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION .

**VIONGOZI WA TAASISI-**Maana yake ni Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mweka Hazina.

**JUMUIYA-** Maana yake ni muungano wa vyama kwa ajili ya kutimiza malengo yaliko kwenye katiba.

**BODI YA WADHAMINI** –itamaanisha wadhamini wa kwanza katika msingi na wadhamini wengine wapya watakao chaguliwa katika jumuiya.

**FEDHA** – itamaanisha fedha yoyote kutoka kwa wanajumuiya au vyanzo vyovyote ambavyo kwayo vitakuwa vikitolewa na shirika kama uwekezaji au mali itakayo wasilishwa kwa kibali.

**IBARA YA 5: UWANAJUMUIYA**

1) **Aina ya wanajumuiya**

a) **WanajumuiyaWanzilishi**
Wanajumuiya wanzilishi ni wale ambao walikuwepo ambapo Taasisi hii inaanzishwa.

b) **Wanajumuiya wa Kujiunga**
Hawa niwanajumuiya ambao watajiunga na Taasisi baada ya kusajiliwa

c) **Wanajumuiya wa Heshima**
Hawa niwanajumuiya ambao wanapewa uanajumuiya kutokana na ushirikiano wanaoutoa kwenye taasisi kama vile kufadhili na kusaidia kwa hali na mali maendeleo ya taasisi.

2) **SIFA ZA MWANAJUMUIYA.**

a) Lazima awe Mwanajumuiya wa kweli.

b) Awe mwaminifu na muadilifu.

c) Awe na Mjasiliamali katika Nyanja yoyote ile ikiwemo kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na uvuvi.

d) Awe raia wa Tanzania.

e) Awe na akili timamu.

f) Mwanajumuiya lazima aweze kujitolea kwa kila hali.

g) Mwanajumuiya lazima awe na miaka kuanzia 18 na awe anakubaliana na masharti ya katiba hii.

h) Mwanajumuiya ni lazima aweze kujitolea kwa ajili ya jumuiya.

i) Awe tayari kujitolea kwa hali na mali.

j) Mwanajumuiya awe tayari kushiriki kufanya makusanyo ya mtaji ya pamoja ilikufanya shughuli za pamoja.

k) Mwanajumuiya awe tayari kuikubali pesa inayotokana na mauzo/kukusanywa kwenye vyanzo vyovyote anavyosimamia/ vilivyokubalika iingie kwenye mfuko wa jumuiya benki, ndipo mgao wake utalipwa kulingangana na makubaliano.

l) Mwanajumuiya akubali kukatwa makato yeyote yatakayokuwa yanamhusu binafsi kutoka kwenye akaunti yake au Jina Lake.

m) Mwanajumuiya atapaswa kutafuta haki zake nje ya jumuiya pale tu atakapokuwa amepitia ngazi zote za jumuiya za kimaadili na ushuruhishi;

n) Awe tayari kuilinda, kuitetea, kuienzi na kuihifadhi katiba ya TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEA)

3) **Haki Za Mwana jumuiya**

a) Kuchagua na kuchaguliwa kwenye uongozi.

b) Kuhudhuria vikao na mikutano ya Taasisi.

c) Kulipa ada za uanajumuiya.

d) Kushiriki kazi zote za TANCEA kwa hali na mali.

e) Kuandikishwa kwenye daftari la wanajumuiyana kupewa kitambulisho.

f) Kuchangia mawazo, kukosoa na kutoa ushauri kwa viongozi.

g) Kila mwanachama atakuwa na haki ya kusikilizwa.

**4) Wajibu wa Mwanajumuiya**

a) Kushiriki katika kutekeleza majukumu mbalimbali katika Taasisi ili kufikia Malengo ya Maendeleo tunayotarajia.

b) Kutangaza Taasisi na shughuli zake.

c) Kuitetea Taasisi popote alipo.

d) Kuzingatia shughuli za Taasisi na kujitolea kwa hali na Mali.

e) Kujiuzulu uanajumuiya endapo mwanajumuiya ameenda kinyume na katiba ya Taasisi.

f) Kutoa ada na Michango ya Taasisi kwa wakati pamoja na kushirikiana na wanajumuiya wenzake kwa hali na Mali.

**5) Ukomo Wa Mwanajumuiya**

a) Kuacha kujitolea kwa hali na mali.

b) Kujiuzulu uanajumuiyawa Taasisi.

c) Kwenda kinyume na katiba hii.

d) Kutokwa na akili.

e) Kushindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya kutoa taarifa rasmi ya maandishi.

f) Kwenda kinyume na sifa za uanajumuiya.

g) Kushindwa kutekeleza kazina majukumu yaliyomo ndani ya Katiba.

**IBARA YA 6: MALENGO NA MADHUMUNI**

Malengo na Madhumuni makuu ya **TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION** ni:

a) Kuwaunganisha wanachama ambao ni wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimba madini, wazee, walemavu, vijana katika shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji, uchimbaji wa madini, Maliasili n.k ili waweze kujiajiri katika umoja wao na wingi wao kwa kiwango cha kisasa cha kiteknohama ili kupata soko la pamoja baada ya kuzalisha na kusindika kwa kutumia viwanda vyenye viwango vya kimataifa;

b) Kuelimisha wanachama katika kutambua haki na wajibu wao katika biashara zao kwa ajili ya kufanya ushindani wa masoko ya ndani na nje ya Tanzania;

c) Kuwa na akaunti ya benki ya pamoja ya jumuiya itakayokuwa inaingiza mapato yote ya mauzo na kutoa malipo yote ya matumizi;

d) Kuhamasisha Wanakikundi ili waweze kuchangia muda na nguvu zao kwa shughuli za Umoja zenye kulenga na kutatua tatizo la umaskini na ajira, kwa hali na mali na kuleta maendeleo Miongoni mwa wanakikundi;

e) Kuchochea maendeleo na kuomba ushirikiano wa kila mmoja wetu kushiriki katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Kikundi na Wanakikundi kwa ujumla;

f) Kubuni na Kuanzisha miradi na kukuza uchumi kwa kutumia fedha za Kikundi kama vile ujasiriamali mbalimbali, kilimo na mifugo;

g) Kuwekeza kwenye biashara kwa lengo la kupata faida ambayo itagawanywa kwa wanakikundi;

h) Kutambuana na kuzungumza kwa njia ya kuleta uhusiano mwema miongoni mwa Wanakikundi;

i) Kuhamasishana miongoni mwa Wanakikundi kutoa michango mbali mbali ya kuimarisha Kikundi;

j) Kusaidiana katika masuala ya kijamii wakati wa shida na raha hasa kwenye mazishi, harusi na maradhi;

k) Ufuatiliaji na utekelezaji wa masuala yote ya Kikundi;

l) Kushirikiana na wadau wa mambo ya Ukimwi ili wawaelimishe wanajumuiya wetu ili waepukane na maambukizi ya magonjwa yanayosababishwa na Virusi vya ugonjwa wa Ukimwi;

m) Kuanzisha, kuendeleza na kusimamia, semina na makongamano;

n) Kuhakikisha umoja huu unakwenda mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, kata hadi vijijini na kuwainua kwa kuwaunganisha wanajumuiya na kuwawezesha wana umoja kwa kuwapa elimu na manufaa ya kufanya maendeleo ya pamoja kwa maslahi yao wenyewe kupitia hali ya tabia nchi na kwa kuchukua maslahi ya vitu vilivyoachwa bila kuendelezwa kama vile mabonde, mito, misitu, maziwa, milima, miamba n.k.

**IBARA YA 7: UONGOZI NA UTENDAJI**

**Kutakuwa na muundo wa uongozi kiutawala kama ifuatvyo:**

**A. Muundo wa uongozi wa Jumuiya**

**a)** Mwenyekiti
**b)** Katibu Mkuu
**c)** Naibu Katibu Mkuu
**d)** Mweka Hazina

**B. Sifa Za Kiongozi**

a) Awe mwanajumuiya wa TANCEA
b) Awe Muaminifu na Muadilifu
c) Awe na Kiwango cha Elimu kuanzia Sekondari au Chuo Kikuu.
d) Awe na Umri kuanzia Miaka 21na kuendelea.
e) Awe na Akili timamu.

1. **Bodi ya Wadhamini**

Kutakuwa na Bodi ya Wadhamini itakayojumuisha:

i. Mwenyekiti wa bodi,
ii. Mwenyekiti Msaidizi,
iii. Katibu Mkuu wa bodi,
iv. Katibu Mkuu Msaidizi,
v. Wajumbe wa bodi,
vi. Mweka Hazina mkuu wa Bodi,
vii. Wajumbe watatu watakao pigiwa Kura kutoka Mkutano mkuu na wajumbe.

**a) Bodi ya wadhamini wajumuiya itakuwa na majukumu yafuatayo:**

I. Bodi ya wadhamini itakuwa na jukumu la kusimamia mali zote za jumuiya zinazohamishika na zisizohamishika
II. Itatekeleza majukumu yake mengine kwa mujibu wa Sheria inayosimamia Bodi ya Wadhamini.

**IBARA YA 8:**

**1. KAZI ZA VIONGOZI WA JUMUIYA**

**a) Mwenyekiti**

i. Atakuwa na madaraka yote ya kuendesha mikutano yote ya TANCEA kwa kipindi chote atakapokuwa madarakani isipokuwa kama atakuwa na matatizo ya kiafya au udhuru hatatakiwa kufanya hivyo;
ii. Atakuwa msemaji mkuu wa TANCEA;
iii. Atatoa taarifa ya utendaji ya mwaka kwenye mkutano mkuu;
iv. Atakuwa msimamizi wa shughuli zote za Taasisi;
v. Ndiye kiongozi mkuu wa Taasisi katika masuala yote ya kiutawala;
vi. Atakuwa miongoni mwa watia saini kwenye nyaraka mbalimbali za Taasisi;
vii. Atakuwa miongoni mwa watia saini kwenye akaunti ya Taasisi;
viii. Atakuwa mwakilishi wa TANCEA ndani na nje ya nchi;

**b) Katibu Mkuu**

i. Atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Taasisi na atasimamia na kuangalia Shughuli zote za Taasisi za kila siku kwa kushirikiana na kamati ya utendaji;
ii. Atakuwa mtunzaji wa kumbukumbu zote za Taasisi;
iii. Ataitisha mikutano yote, ikiwemo Mkutano mkuu kwa kushauriana na Mwenyekiti;
iv. Atakuwa mwandishi wa mihutasari kwenye mikutano yote ya Taasisi;
v. Atakuwa msomaji wa mihutasari yote ya Taasisi kwenye mikutano;
vi. Atahakikisha kuwa maazimio yote pamoja na maelekezo ya mkutano mkuu yanatekelezwa kama ilivyopangwa;
vii. Atakuwa kiungo cha mawasiliano kwa niaba ya Taasisi kuandaa na kuwasilisha ripoti mbalimbali katika mkutano mkuu;
viii. Atakuwa miongoni mwa watia saini kwenye akaunti ya Taasisi;

**c) Naibu Katibu Mkuu**

i. Atafanya kazi zote za Katibu Mkuu pale ambapo katibu Mkuu atakuwa na Dharura yoyote.

**d) Mweka Hazina Mkuu**

i. Atakuwa mtunzaji na mlinzi wa kumbukumbu zote kuhusiana na maswala yote ya fedha za Taasisi na atatunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya Taasisi;
ii. Atasimamia utayarishaji Bajeti ya mwaka ya Taasisi, atasimamia, kufuatilia na kuangalia matumizi ya Taasisi kwa kushirikiana na wajumbe wa Kamati ya Utendaji;
iii. Atakuwa ni miongoni mwa watia saini kwenye akaunti ya Taasisi;
iv. Atasimamia utayarishaji wa urari wa hesabu kwa madhumuni ya ukaguzi wa fedha;
v. Atasimamia uandaaji bajeti ya mapato na matumizi na ambayoitawasilishwa katika mkutano mkuu wa mwaka;
vi. Atawasilisha maelezo ya mapato na matumizi ya fedha kwenye mkutano mkuu wa mwaka;
vii. Ataidhinisha malipo yote ya Taasisi kwa Ruhusa ya Mwenyekiti.

**2. Kamati Utendaji**

Kamati tendaji itaundwa na viongozi wa jumuiya na wajumbe saba watakaochaguliwa na mkutano mkuu.

(a) Kamati itakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitatu na itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu kuangalia kwa kina maswala yanayohusiana au yatokanayo na utekelezaji wa Shughuli za kamati.
(b) Kamati inaweza kuteuwa mmoja wa wanakamati kuwa katibu ili kuendesha Shughuli za ukatibu kwa kamati.
(c) Kikao cha kamati ya utendaji kitakuwa halali kwa kuhudhuriwa na zaidi ya nusu ya wajumbe wote.
(d) Sifa zitakiwazo kuchaguliwa viongozi zitatumika pia kwa wajumbe wa kamati ya utendaji.

**Kazi ya kamati ya tendaji itakuwa Kama Ifuatayo:**

i. Itakuwa na majukumu ya kutekeleza maazimio ya mkutano mkuu, kusimamia uboreshaji wa huduma kwa maslahi ya Taasisi pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Taasisi.
ii. Itahusika na ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi, kadhalika.
iii. Itasimiamia na kufuatilia kwa karibu Shughuli za kila siku za Taasisi ikiwemo matumizi bora ya fedha na uimarishaji wa miundombinu na majengo.
iv. Kuhakikisha amani, mshikamano, utulivu na heshima inadumishwa.
v. Kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu kwa kupendekeza miundo na njia za kufanikisha utekelezaji wake wa Taasisi.
vi. Kamati ina mamlaka ya kuteuwa idara ndogondogo miongoni mwa wajumbe au kutaka wanajumuiya wengine kufanya hivyo.
vii. Kuulizia/kuhoji hoja yeyote kwa niaba ya kamati na Kuendesha baadhi ya Shughuli za Taasisi kama itakavyoelekezwa na viongozi.

**3. Ukomo waViongozi.**

a) Kuisha Muda wa Uongozi kwa Mujibu wa Katiba Miaka Mitatu.
b) Kutoka katika Jumuiya ya TANCEA.
c) Kukiuka Maadili ya Uongozi kwa Misingi ya Katiba hii.
d) Kutokuwa Muaminifu na Muadilifu katika Ulinzi wa Mali za Taasisi.
e) Kifo.
f) Kujitoa / Kuacha Uongozi kwa hiyari yake.

**4. Muda Wa Viongozi Kukaa Madarakani**

Kwa Mujibu wa Katiba hii Viongozi watakaa Madarakani kwa muda wa Miaka Mitatu (3) na anaweza akachaguliwa tena baada ya muda huo.

**IBARA YA 9: KAMATI NA IDARA ZA TAASISI**

Kutakuwa naKamati na idara mbalimbali katika Taasisi kama ifuatavyo:

**1) Kamati ya Utendaji**

a) Kutakuwa na kamati ya utendaji itakayoundwa na watu wasiopungua watatu na wasiozidi watano ambao watateuliwa na viongozi,miongoni mwa viongozi wa kawaida na wanajumuiya waliojitolea ambao watatoka kwa hiyari yao kutoa huduma kwa maslahi ya Jumuiya na maendeleo ambayo majina yao yatawasilishwa kwenye mkutano mkuu kwa ajili ya uchaguzi.
b) Wajumbe wa kamati ya utendaji watachaguliwa miongoni mwao meneja na mwekahazina na atathibitishwa kwa kura za wanajumuiya.
c) Kamati itakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitatu na itakutana mara moja kila baada ya mwezi mmoja kuangalia kwa kina maswala yanayohusiana au yatokanayo na utekelezaji wa Shughuli za kamati.
d) Kamati inaweza kuteuwa mmoja wa wanakamati kuwa katibu ili kuendesha Shughuli za ukatibu kwa kamati.
e) Kikao cha kamati ya utendaji kitakuwa halali kwa kuhudhuriwa na zaidi ya nusu ya wajumbe wote.
f) Sifa zitakiwazo kuchaguliwa viongozi zitatumika pia kwa wajumbe wa kamati ya utendaji.
g) Kazi ya kamati ya utendaji itakuwa Kama Ifuatayo:
   i. Itakuwa na majukumu ya kutekeleza maazimio ya mkutano mkuu, kusimamia uboreshaji wa huduma kwa maslahi ya Taasisi pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Taasisi.
   ii. Itahusika na ukusanyaji wa michango na kadhalika.
   iii. Itasimiamia na kufuatilia kwa karibu Shughuli za kila siku za Taasisi ikiwemo usafi na uimarishaji wa jengo na majengo mengine ambayo ni ya Taasisi.
   iv. Kuhakikisha amani, mshikamano, utulivu na heshima inadumishwa.
   v. Kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu kwa kupendekeza miundo na njia za kufanikisha utekelezaji wake wa Taasisi.
   vi. Kamati ina mamlaka ya kuteuwa idara ndogondogo miongoni mwa wajumbe au kutaka wanajumuiya wengine kufanya hivyo:Kuulizia/kuhoji hoja yeyote kwa niaba ya kamati na Kuendesha baadhi ya Shughuli za Taasisi kama itakavyoelekezwa na viongozi.

**2) Idara ya Fedha,Uchumi na Mipango**

a) Kutakuwa na idara ya Fedha,Uchumi na mipango ambayo itawajibika katika kamati ya utendaji.

b) Kamati ya utendaji itaitisha mkutano wa Fedha,uchumi na mipango na watawachagua viongozi wao,Katibu,Mweka Hazina,Mwanasheria,Mwanataaluma na wajumbe watatu.
c) Idara itatengeneza sheria na kanuni bora kwa ajili ya idara ya Fedha,uchumi na mipango.
d) Kamati ya utendaji inaweza kuivunja idara hii ya Fedha,uchumi na mipango Kama itaenda kinyume na misingi ya katiba hii.

**3) Kamati ya nidhamu**

Kutakuwa na kamati ya nidhamu ambayo itaundwa na wajumbe wasiopungua watano na watateuliwa na mkutano mkuu na kazi yake itakuwa kusimamia nidhamu ya wanajumuiya pamoja na kutatua migogoro katika ngazi ya awali.

**IBARA YA 10: UCHAGUZI**

Kutakuwa na uchaguzi kila baada ya miaka mitatu kwa utaratibu ufuatao:

**(a) Taratibu za Uchaguzi**

i. Kutakuwa na Kamati Maalum ya kusimamia uchaguzi itakayoteuliwa na mkutano mkuu wa wanajumuiya.

**(b)Utaratibu wa Kupiga Kura**

i. Kutakuwa na fomu kwa wagombea wote wa nafasi za uongozi ambapo zitachukuliwa na kurejeshwa kabla ya uchaguzi kwa wiki mbili na kura zitapigwa kwa siri;
ii. Mshindi atapatikana kwa kupata kura nyingi zaidi ya mwenzake;
iii. Kura zikigongana Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi atakuwa na kura ya veto;
iv. Washindi watapewa Vyeti vya Ushindi kwa Nafasi walizopata na Kamati ya Uchaguzi.

**IBARA YA 11: MIKUTANO**

**1) Aina za Mikutano**
a) Mkutano Mkuu
b) Mkutano Mkuu Maalum
c) Mkutano wa Kawaida
d) Mikutano ya kamati tendaji wa kila mwezi

**2) Taratibu za kila mkutano**

**a) Mkutano Mkuu.**

i. Kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa Taasisi ambao utafanyika ndani ya **TANCEA** mara moja kwa mwaka kwa muda na tarehe kama itakavyopangwa na Mwenyekiti na katibu wa TANCEA.

ii. Kutakuwa na taarifa ya kufanyika Mkutano mkuu wa mwaka kwa muda wa siku 28 kabla ya kufanyika Mkutano mkuu , mkutano mkuu utaitishwa na katibu Mkuu kwa kushirikiana na Mwenyekiti;

iii. Mkutano Mkuu utakuwa halali kwa kuhudhuriwa na Theluthi mbili (2/3) ya wanajumuiya wote.

iv. Mkutano Mkuu ukiitishwa kwa mara ya kwanza isipotimia akidi ya theluthi mbili (2/3) mara ya pili ukiitishwa wajumbe wakiwa Nusu ya wanajumuiya watakuwa na uhalali wa kufanya mkutano Mkuu na Maamuzi yatakayofikiwa yatakuwa ni halali

**(b) Mkutano Mkuu Maalum**

i. Mkutano maalum unaweza kuitishwa wakati wowote kwa mwaka itakapobainika kuwa kuna haja nzito na nyeti ambazo hazitataka kusubiri mkutano wa mwaka ambapo utahitaji udharura wa suluhisho;

ii. Mkutano Mkuu Maalum utakuwa halali kwa kuhudhuriwa na Nusu (1/2) ya wanajumuiya wote.

**c )Mkutano wa Kawaida**

i. Mkutano wa kawaida utaitishwa na Mwenyekiti na kuusimamia kwa kushauriana na katibu kwa wakati wowote ule kama itatokea dharura ambayo haitahitaji kusubiri mkutano mkuu.

ii. Mkutano wa kawaida utakuwa halali ukihudhuriwa na wajumbe wasiopungua Nusu (1/2) waliosajiliwa katika daftari la wanajumuiya

**d) Mkutano wa Kamati Tendaji wa Kila mwezi;**

i. Huu utakuwa ni mkutano utakaowashirikisha wajumbe wasiozidi theluthi mbili (2/3) ya viongozi ambao huchaguliwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka ambao ni mwenyekiti, mwenyekiti msaidizi, katibu, katibu msaidizi, mweka hazina pamoja na wajumbe wa kamati tendaji watakaochaguliwa kwenye mkutano mkuu;

**3. Kazi za Mikutano**

**a) Mkutano Mkuu**

i. Kupokea na Kupitisha muhtasari wa Mkutano uliopita.
ii. Kuthibitisha taarifa ya fedha na ripoti zingine za maendeleo.
iii. Kutoa na kupitisha maamuzi ya miradi ya maendeleo.
iv. Kupanga dira ya maendeleo na kupitisha mikakati ya uendeshaji.
v. Kupokea na kujadili taarifa kutoka kwa Mwenyekiti na taarifa nyinginezo kutoka katika Kamati ya utendaji.
vi. Kupokea taarifa na maelezo ya matumizi ya fedha kutoka kwa mweka hazina ikiwemo taarifa inayohusu mapato na matumizi na kujadili.
vii. Kupokea taarifa za utendaji na maendeleo kutoka kwa katibu na kuipitisha.
viii. Kuchagua viongozi inapotakiwa kufanya hivyo.
ix. Kufanya marekebisho ya katiba kama itahitajika kufanya hivyo.
x. Kumwondoa mjumbe yeyote wa kamati ya utendaji.
xi. Mengineyo Kama itakavyoruhusiwa na Mwenyekiti.

**b) Mkutano Mkuu Maalum**

i. Mabadiliko ya katiba.
ii. Kujaza nafasi mbalimbali za viongozi.
iii. Kujadili swala lolote la kipekee ambalo halitasubiri mkutano mkuu wa mwaka.

**c) Mkutano wa Kawaida**

i. Mabadiliko ya katiba.
ii. Kujaza nafasi mbalimbali za viongozi
iii. Kujadili mambo mengine yatakayojitokeza kwa idhini ya Mwenyekiti.

**d) Mkutano wa Kamati Tendaji wa Kila mwezi**;

i. Kamati ya utendaji ndiyo itakayosimamia utendaji na kutoa maelekezo na taratibu zake kwa wanajumuiya wa kikundi hiki kwa kuainisha shughuli/majukumu mengine ya kamati ya utendaji;

ii. Kupokea maombi ya wanakikundi wanaotaka kujiunga na kuyajadili;

iii. Kuangalia shughuli zote za kikundi pamoja na kuangalia mienendo ya kikundi na viongozi wake;

iv. Kusimamia matumizi yote ya kikundi pamoja na kuandika mihutasari ya majadiliano na maazimio yote ya mikutano ya kikundi;

v. Kumsimamisha kiongozi au mwanakikundi yeyote atakayepatikana na kosa, baada ya kupatikana na kosa shauri hilo litapelekwa kwa wanakikundi wote kwenye mkutano mkuu kwa maamuzi ya mwisho;

vi. Itasimamia matumizi ya fedha, vifaa na mali nyingine za Jumuiya;

vii. Itakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni na taratibu za kuendesha kikundi;

viii. Itapokea maoni na mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wanajumuiya na kuyawakilisha kwenye mkutano mkuu;

ix. Itatengeneza mifumo ya uendeshaji wa shughuli za jumuiya pamoja na kutengeneza mahesabu ya jumuiya, kusimamia ukaguzi wa mahesabu na kuyawakilisha kwenye mkutano mkuu;

x. Itafanyia kazi shughuli zote halali kulingana na madhumuni ya jumuiya na inaweza kuunda kamati nyingine ndogondogo kama itahitajika ili kufanikisha malengo ya jumuiya;

xi. Kujadili wabia wapya;

xii. Kujadili miradi mipya;

xiii. Kujadili kuhusu maafa kwa wanakikundi;

xiv. Kamati ya utendaji itakutana mara moja kila mwezi,Jumapili ya kwanza ya mwezi unaofuata au kama itakavyoamuriwa na kwa sababu zitakazo jitokeza.

**IBARA YA 12: MASUALA YA FEDHA NA MWAKA WA FEDHA NA USIMAMIZI WA FEDHA**

1) TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION TRUST itakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo;-

a) Viingilio kwawanajumuiya wapya.
b) Ada za uanajumuiya.
c) Michango mbalimbali kutoka kwa waumini.
d) Michango ya misaada toka Kwa wahisani mbalimbali wa Ndani na Nje ya Nchi.
e) Kilimo na mifugo.
f) Biashara mbalimbali zinazokubaliana na maadili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 2) MWAKA WA FEDHA

Mwaka wa fedha waTANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION utaanzia mwezi Januari na kuishia Disemba kwa kila Mwaka.

## 3) USIMAMIZI WA FEDHA

a) Taasisi hii kama zilivyo Taasisi zingine inayozalisha na kutumia fedha inalazimika kushikamana na kufuata kikamilifu utaratibu na kanuni za fedha katika kukusanya, kuhifadhi,kutunza na kutumia fedha kwa kufuata njia za usalama wa fedha kama zinavyoelekezwa na taaluma ya uthibiti wa fedha na nyaraka za fedha.

b) Mtunza hazina atahakikisha kuwa kuna "safe"maalum za kuhifadhi fedha zinazo kusanywa kupitia miradi ya Taasisi kabla ya kuzipeleka benki pia kuzihifadhi kutoka benki kabla ya kuzitawanya kwa ajili ya malipo mbalimbali yaliyoidhinishwa.

## 4) UENDESHAJI WA AKAUNTI

Kutakuwa na waendeshaji wanne ambao watakuwa na mamlaka ya kuendesha akaunti ya Taasisi Wawili ni Mwenyekiti na Mweka hazina wa Taasisi na Wajumbe wawili watakao teuliwa na Wanajumuiya,Kila kundi litakuwa na Muwakilishi mmoja katika utoaji wa fedha akiwemo Mweka hazina.

a) Malipo ya fedha yatafanyika baada ya kuidhinishwa na maafisa waliopewa mamlaka na Taasisi,baada ya kuhakikishwa kuwa hati za malipo hazina wasiwasi wowote juu ya uhalali na kuwa zina sifa zote zinazohitajika kulingana na sheria za fedha.

b) Mabadiliko ya saini za benki yatafanyika pale tu inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwa lengo la kulinda na kudhibiti usahihi wa akaunti ya fedha za Taasisi.

c) Taasisi italazimika kutengeneza hesabu za uwiano za mwezi kati ya mahesabu ya TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION yanayoonyeshwa kwenye vitabu vyao ili kupata usahihi kiasi cha fedha ambacho Taasisi iliweka na kukichukua katika mwezi huo hatimaye kupata baki ya fedha zilizokuwepo benki.

d) Mtunza hazina atalazimika kutoa ripoti ya tofauti za kimahesabu alizozigundua kupitia nyaraka za fedha haraka iwezekanavyo ili kuweza kudhibiti uharibifu mapema atatoa ripoti hii kwa uongozi husika na si vinginevyo.

e) Wakaguzi wataitwa ili kukagua mahesabu ya Taasisi kila ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha wa Taasisi ili kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanywa, upokeaji wa fedha kupitia vyanzo vya Taasisi.

f) Mwisho wakaguzi watatoa taarifa kwa utawala na kutoa maelekezo juu ya tofauti zozote zinazotokana na ubadhirifu na makosa ya kiufundi katika vitabu vya mahesabu na kutoa taarifa mapema juu ya njama za majaribio na kupitia sehemu mbalimbali ili kukinga hasara inayoikabili Taasisi.

g) Kwa vile mahesabu ndio sehemu muhimu kwa uhai wa Taasisi pamoja na ukaguzi wa wataalamu wa fedha uongozi unalazimika kuwasiliana na Taasisi mbalimbali ili kupata ufanisi wa kuzalisha kupokea,kulinda na kutumia fedha za Taasisi.

**IBARA YA 13: MUHURI**

Kutakuwa na mhuri wa Taasisi utakaosomeka kwa jina laTANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEA) ambao utagongwa katika nyaraka zote muhimu za **TANCEA**, Muhuri huu wa Taasisi utakuwa chini ya uangalizi wa Katibu Mkuu na utagongwa akishuhudia.

**IBARA YA 14: MABADILIKO YA KATIBA**

a) Katiba hii itabadilishwa wakati wowote Kama itahitajika kufanya hivyo.
b) Katiba hii itafanyiwa marekebisho Kwa kuungwa mkono na wajumbe wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya wajumbe waliosajiliwa katika daftari la wanajumuiya.
c) Katiba hii itafanyiwa marekebisho kwenye Mkutano mkuu, Mkutano maalumna Mkutano wa kawaida.
d) Mikutano itahudhuriwa nawanajumuiya, viongozi, kamati ya utendaji na wageni waalikwa.

**IBARA YA 15: KUVUNJIKA KWA TAASISI**

1) Si malengo ya kuanzisha Jumuiya hii ili uvunjike, hivyo,si matarajio ya wanachama kuwa Jumuiya hii utavunjika.
2) Bila kuathiri ibara ya 15(1) Jumuiya hii unaweza kuvunjika kwa sababu zifuatazo:-

   a) Serikali ikiamua kuuvunja.
   b) Mgogoro usiotatulika ndani na nje ya Jumuiya.
   c) Wanachama kupungua mpak kufikia chini ya kumi (10)
   d) Maamuzi ya 2/3 ya kura za wajumbe kwenye Mkutano Mkuu kupitisha maamuzi ya kuvunja Jumuiya.

3) Endapo Jumuiya hii utavunjika mali zote zitabaki chini ya uangalizi wa Bodi ya wadhamini ambayo itafanya yafuatayo:-
    a) Kukusanya madeni ambayo Jumuiya kama Jumuiya unadai kama yapo.
    b) Kulipa madeni ambayo Jumuiya unadaiwa kama yapo.
  a) Baada ya kukusanya na kulipa madeni, mali na fedha zitakazobaki baada ya migawanyo tajwa hapo juu zitatolewa na kugawanywa kwa Taasisi zingine na mashirika ya misaada ambazo zitaonekana zina malengo sawa na Taasisi kwa kukubaliana na wanajumuiya.

**IBARA YA 16: TARATIBU ZA KUTATUA MIGOGORO**

Migogoro ndani ya Jumuiya hii itatatuliwa kwa utaratibu ufuatao:-

a) Migogoro itaanzia kwenye kamati nidhamu ya Jumuiya ambayo utaundwa na wanachama wasiozidi watano na watateuliwa na mkutano mkuu kwa ajili ya utatuzi.
b) Migogoro isiyomalizwa kwenye kamati nidhamu itapelekwa kwenye kamati tendaji, ambayo itatoa maamuzi yake juu ya migogoro hiyo.
c) Mgogoro isiyomalizwa kwenye kamati tendaji itapelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa Jumuiya.
d) Endapo mmoja wapo kwenye mgogoro huo atakuwa hajaridhika na maamuzi yoyote yaliyotolewa ndani ya Jumuiya basi atakuwa na haki ya kwenda Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii Wizara ya mambo ya ndani ya nchi kwa ajili ya utatuzi.
e) Kama Msajili wa Jumuiya za Kijamii atashindwa kutatua mgogoro huo, mgogoro huo unaweza kupelekwa mahakamani.

**IBARA YA 17:UHUSIANO**

Taasisi itakuwa na uhusiano na Jumuiya yeyote ya Kitaifa au Kimataifa ambayo inajihusisha na mambo ya kijamii na maendeleo ambayo yenye malengo, madhumuni yanayo endana na Taasisi yetu kwa mujibu wa katiba hii.

**IBAYA YA 18: BODI YA WADHAMINI**

Kutakuwa na bodi ya wadhamini ambayo itaundwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi saba ambao watachaguliwa na Mkutano mkuu, kazi ya bodi ya wadhamini itakuwa kusimamia mali za jumuiya hii.

**IBARA YA 19: ITHIBATI YA KATIBA**

Katiba hii imepitishwa na kuthibitishwa na wanajumuiya wote waliohudhuria mkutano Mkuu leo hapa Dar-es-Salaam, tarehe...............mwezi..............mwaka................